

TAARIFA YA SHULE MPYA YA MABWE TUMAINI GIRLS HIGH SCHOOL.

Katika kutekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2015 **sura ya nne,kifungu na 52 (b)(i) ukurasa 97** serikali ya CCM iliahidi kusimamia utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 kwa kuhakikisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano **(2015-2020)** asilimia 20 ya wahitimu wa elimu msingi wanaendelea na masomo katika ngazi za sekondari ya juu.Kwa kuzingatia hayo wilaya ya kinondoni ilianzisha ujenzi wa shule ya sekondari ya juu(A-Level) kwa ajili ya wasichana ambao wana idadi kubwa zaidi ya wahitimu kuliko wa kiume. Kwa kipindi chote hicho cha nyuma wilaya ya Kinondoni haikuwa hata na shule moja ya kidato cha tano na sita inayomilikiwa na serikali hivyo iliweka msukumo wa kipekee katika ujenzi wa shule hii.

Shule ya sekondari ya Mabwe Tumaini Girls ni mradi uliojengwa na wilaya ya Kinondoni kwa kushirikiana na wadau "**Goodneighbors**" kwa Lengo la kuimarisha huduma za elimu ya kidato cha tano na sita kwa watoto wa kike.Hatua hii imefanyika ili kuwapa nafasi watoto wa kike kupata elimu na kuawepusha na changamoto za kutembea mwendo mrefu kufuata shule, mimba za utotoni na kukosa elimu.Ujenzi umefanyika katika kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ya kuwalinda na kuwawezesha watoto wa kike ili baadae nao waweze kulitumikia taifa lao kikamilifu. Mradi huu kwa sasa unajumuisha miundombinu ya majengo yafuatayo; Madarasa sita (6), Maabara tatu (3), Bweni moja (1), Ofisi ya Walimu moja (1), Bwalo (1), Ukuta kuzunguka Shule na Nyumba za Walimu 4 kwa kuanzia.

Shule hii ilipata usajili wake wenye namba **S.5221** tarehe **2.4.2019** na imeanza kupokea wanafunzi kwa mara kwanza. Hadi kufikia tarehe **18.7.2019** jumla ya wanafunzi **83** wamelipotika kati ya wanafunzi **123** waliochaguliwa kujiunga na shule hii.Shule hii ina tahsusi za sayansi na sanaa ambazo ni "**PCB,PCM** na **HKL**".Idadi ya walimu waliopo ni **13** ikiwa walimu wa kiume ni **06** na wa kike **07**

Mradi huu wa Ujenzi wa Shule ya sekondari ya Mabwe Tumaini Girls umefanyika kwa awamu mbili.Awamu ya kwanza iligharimu kiasi cha **Shilingi 1,269,468,952.55** na awamu ya pili ilitumia kiasi cha **Shilingi 127,531,825.00** .Hivyo basi mradi wote kwa sasa umekuwa na gharama ya **Shilingi 1,397,000,777.55**.

Shule ya Sekondari ya Mabwe Tumaini Girls ni kati ya miradi ya mwenge iliyopitiwa mwaka **2018** na kuwekewa jiwe la Msingi. Shule kwa wakati huo ilikuwa na Majengo **11** ambayo ni Nyumba 03 za walimu,Madarasa 04,Maabara 01,Bweni la wanafunzi,Bwalo la chakula na Ofisi ya walimu. Kwa miundo mbinu hiyo iliyokuwepo yalitolewa maagizo na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa wakati huo kwa Wilaya kuongeza Miundo mbinu mingine ili kukamilisha mahitaji halisi ya shule ikiwa ni kufanya Ujenzi wa maabara 02,Madarasa 02,Kuweka Umeme na Maji. Katika kutekeleza maagizo haya Wilaya ilitenga na kutumia jumla ya **shilingi 127,531,825.00** kama ifuatavyo;

- I. Kiasi cha **Shilingi 100,000,000.00** zimetengwa na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa **02** na Maabara **02** na ujenzi wake unaendelea na **Shilingi 58,000,000.00** zimetengwa kwa bajeti ya **2019/20** kwa ajili ya umaliziaji na tunatarajia kukamilisha ujenzi huu mwezi Agosti,2019.
- II. Kiasi cha **Shilingi 24, 838,125.00** zimetengwa na kutumika kwa ajili ya uingizaji umeme kwenye nyumba za walimu,Madarasa,bweni la wanafunzi na uwekaji wa nguzo **06** za umeme toka TANESCO kazi hii imekamilika.

- III. Kiasi cha **Shilingi 2,693,700.00** imetumika kwa ajili ya usambazaji wa maji maeneo yote ya shule ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu, bweni la wanafunzi, ofisi za walimu na vyooni kazi hii imekamilika.

PICHA YA SHULE YA MABWE TUMAINI GIRLS HIGH SCHOOL

